## *KAGERA COOPERATIVE UNION (1990) LIMITED*

KCU
QUALITY
COFFEE
*Kagera Cooperative Union*

**TAREHE 10.02.2026**

**TANGAZO LA ZABUNI YA KUPANGISHA HOTELI YA BUKOBA COOP ILIYOPO CUSTOM ROAD- BUKOBA MANISPAA.**

***Imetangazwa tena***

Kagera cooperative union (1990) LTD (KCU (1990) LTD) inawatangazia wananchi wote, watu binafsi na makampuni ya ndani nan je ya nchi kuomba zabuni ya kupangishwa Hotel ya Bukoba Coop iliyopo viwanja No. 189, 190, 192, na 193 Block LDA Custom Road- Bukoba Manispaa. Eneo linatumika kwa matumizi ya Hoteli kwa maana ya vyumba, mgahawa, majiko, sehemu za mikutano na sherehe mbalimbali, Baa na eneo la kuegesha magari. **Ili kuona mandhari ya Hotel hii tembelea Link: https://kcu.or.tz/bukoba-coop-hotel/**

**MASHARTI YA ZABUNI**

1. Mwombaji ataje kodi ya kupangishwa kwa mwezi.
2. Mwombaji anatakiwa kulipa ada ya zabuni kiasi cha Tsh 150,000 ambayo haitarudishwa. Fedha zilipwe katika benki ya CRDB akaunti no **01J1055955002 -Kagera cooperative Union, General Account**
3. Mwombaji atapewa nyaraka za maombi zinazopatikana katika ofisi ya manunuzi baada ya kulipa ada ya zabuni siku za kazi kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa saa 2.30 asubuhi hadi 10.00 alasiri.
4. Mwombaji anatakiwa kuomba kupangishwa hoteli hii baada ya kusoma na kuelewa hadidu za rejea ambazo zinapatikana ofisi ya manunuzi baada ya kulipia ada ya zabuni.
5. Mwombaji atatakiwa kutumia jengo hili kwa matumizi ya Hotel tu na si vinginevyo.
6. Mwombaji atawajibika kulinda mali za KCU (1990) LTD atakazokabidhiwa ikiwa ni pamoja na kutunza jengo na mazingira yake katika hali ya unadhifu.
7. Mwombaji anapaswa kuwa na viambatisho vifuatavyo: -
    - Leseni hai ya biashara
    - Kitambulisho cha mlipa kodi (TIN Namba)
    - Kama ni mtu binafsi wasifu wake uambatishwe na picha binafsi ya passport.
    - Kama ni kampuni mwombaji aambatishe hati ya kujasiliwa BRELLA.



CamScanner

9. Maombi yaletwe kwa mkono yakiwa yamefungwa vizuri kwenye bahasha na kufikishwa ofisi ya manunuzi KCU (1990) LTD. Mwisho wa kuleta maombi ni siku ya Jumanne Tarehe 24.02.2026 saa nne kamili asubuhi. **Juu ya bahasha paandikwe "*MAOMBI YA KUPANGISHWA HOTELI YA BUKOBA COOP*".** Ufunguzi wa barua zote utafanyika muda na siku hiyo na waombaji wanaweza kuhudhuria wakati wa ufunguzi.

10. Siku ya kutembelea hoteli inayopangishwa ni tarehe 17.02.2026 saa 4.00 asubuhi siku ya Jumanne. Waombaji wawe wamefika ofisi kuu KCU (1990) LTD muda huo tayari kuondoka kwa pamoja kwenda kwenye hoteli inayopangishwa.

11. Barua zote za maombi ziandikwe kwa anuani ifuatayo: -

***MENEJA MKUU,***
***KCU 1990 LTD,***
***BOX 5,***
***BUKOBA.***

KAGERA CO-OPERATIVE UNION (1990) LTD.
P.O. Box 5
10 FEB 2026
BUKOBA

Imetolewa na:-

**MENEJA MKUU**
**KCU (1990) LTD**



CamScanner